# Miktadha ya Matumizi ya U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania

**Gervas A. Kasiga**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dodoma**

kassiga@gmail.com

**Ikisiri**
Tasnia ya Muziki wa Kizazi Kipya wa Kiswahili nchini Tanzania imetekwa na utamaduni wa nje, hususani wa Kinigeria. Hali hii ikiendelea itapoteza utambulisho wa Kitanzania katika sanaa. Kwa hali hiyo, makala imechunguza miktadha ya matumizi ya U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania ili kubaini misukumo yake na kutazama njia za kuupunguza na kuuondosha. Makala imetumia mkabala wa kitaamuli. Data zilikusanywa maktabani na uwandani. Nadharia ya Uhalisia ilitumika kama kiunzi cha uchambuzi na mjadala. Hatimaye, makala imebaini miktadha saba ya utumiwaji wa U-Nigeria. Miktadha hiyo imehusisha mivuto ya kiubidhaishaji, matumizi ya vyombo vya habari, mivuto ya kiujumi na kibunifu, na mivuto kutokana na mwigo kutoka wasanii nguli. Miktadha mingine imehusisha misukumo ya wasikilizaji na watazamaji, ukosefu wa alama ya utambulisho wa kitamaduni, na ukosefu wa elimu ya tasnia ya muziki. Mwisho, imependekezwa kuwa ili kulinda utamaduni wa Kitanzania kupitia muziki, ni vema wasanii wapatiwe warsha, semina, na madarasa maalumu ya kukuza vipaji vyao kwa maslahi ya jamii nzima ya Watanzania.

**Dhana za Msingi**: U-Nigeria, kizazi kipya, muziki, nyimbo, muktadha

## Utangulizi

Dhana ya U-Nigeria imetumika kuhusisha hali ya utayarishaji wa filamu nchini Nigeria ambao, kwa kiasi kikubwa, unahusisha maisha na tamaduni za jamii zilizomo katika nchi hiyo. Tamaduni hizo zinahusisha jamii kubwa tatu ambazo ni za Wahausa, Wayorùbá na Waigbo (Falola, 2003). Pia, dhana ya U-Nigeria inajumuisha filamu za video na video za nyimbo za muziki za Kitanzania zenye kufuata ruwaza ya motifu na mitindo ya utayarishaji wa filamu za Kinigeria. Ruwaza hizo za motifu na mitindo ya Kinigeria huenda sambamba na uchotaji wa maudhui yanayopatikana katika filamu hizo (Haynes na Onookome, 2000; Kasiga, 2013). Aghalabu, katika video hizo, U-Nigeria hujipambanua kupitia mavazi, miondoko ya kiuchezaji, mandhari, utumiwaji wa vifaa vya kiutendaji, matumizi ya jukwaa, matumizi ya lugha, ala, pamoja midundo ya muziki inayoleta ishara za kifasihi.

Video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, kama zilivyo fani nyingine za kifasihi, hutarajiwa kubeba tajriba zinazoambatana na mazingira na utamaduni wa jamii wa video hizo (Jengo na Wenzake, 1982). Hata hivyo, uzoefu unaonesha kuwa, kutokana na utandawazi, video hizi zimekuwa zikionekana kugubikwa na utamaduni wa nje. Utamaduni huu wa nje umekuwa ukijipambanua kutoka kwenye U-Marekani, U-Kongo na kwenye U-Nigeria (Mrikaria, 2007). Ukiondoa lugha ya Kiswahili inayotumika kwenye video hizo, hali ya kuchotwa na utamaduni wa kigeni inazifanya video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kukosa alama nyingine za kisanaa na kitamaduni zenye kuitambulisha jamii ya Kitanzania (Kasiga, 2021). Aghalabu, athari hizo zimetokana na dhana ya utandawazi iliyochukua kani kutokana na ukuaji wa sayansi ya teknolojia (Samwel, 2015).

Mrikaria (2007:202 - 203) alipokuwa anachunguza uibukaji wa teknolojia na athari za utandawazi katika fasihi simulizi nchini Tanzania, alieleza kuwa:

> Teknolojia mpya inaenda sambamba na utandawazi ambao ndani yake kuna udhalilishwaji wa nchi za ulimwengu wa tatu kama Tanzania. Hivyo, utakuta kuwa nafasi ya fasihi simulizi ya nchi zinazoendelea kama Tanzania katika teknolojia ni finyu katika kujitangaza. Mafanikio haya ya kisayansi na teknolojia mpya, yameleta athari kubwa sana katika fasihi simulizi hususani katika utamaduni, mila na desturi zetu. Amali hii ambayo ni utajiri mkubwa wa taifa lolote lile ni muhimu sana katika nchi ….

Kimsingi, maelezo ya Mrikaria yanamaanisha kwamba jamii inayopokea sanaa kutoka nje, kwa kiasi kikubwa, hujikuta ndani ya kiu kubwa ya kubugia tamaduni za watu wengine. Papo hapo, wakati jamii ikiwa inazamia kuzijua tamaduni za watu wengine, hujikuta tayari imeshabadilisha mwenendo na mwelekeo wake (Kasiga, 2021). Hatimaye, mwenendo na mwelekeo wa taifa hupata athari kisiasa, kijamii, kiutamaduni, kisaikolojia, na kiitikadi. Hivyo, wajamii hususani vijana hujikuta wamo ndani ya mwigo wa tamaduni, mila na desturi za mataifa mbalimbali na kuathiri maadili na ustawi wa taifa.

Kinadharia, msanii ndani ya jamii ana wadhifa mkubwa wa kutekeleza matakwa ya jamii yake. Anapounda kazi ya sanaa, huwa na azma ya kuwasiliana na hadhira yake. Kazi yake haiwezi kujitenga na matatizo halisi ya jamii yake; vinginevyo, atashindwa kuyaonesha matatizo, kusaidia kutoa utatuzi na kuamsha ari na moyo wa watu wake (Msokile, 1993). Halikadhalika, nguvu ya usanii hutokana na uzoefu wa msanii katika mazingira yake na kiwango cha ufahamu wake. Kwa ujumla, umuhimu wa

kazi ya sanaa kwa jamii hutokana na jinsi msanii anavyohusisha usanifu wake na matukio muhimu yanayomzunguka. Usanaa wake hubeba ukweli ikiwa umeakisi vizuri uhusiano wa mtu na ukweli wa asili na wa kijamii (Madumulla, 1993). Hivi sasa, kutokana na utandawazi na upokezi mkubwa wa sanaa za nje hususani video za nyimbo za muziki wa Kinigeria, zimeleta mwigo kwa watayarishaji wa video za nyimbo za kizazi kipya.

Hali ya kutokupatiwa thamani kwa utamaduni katika ujenzi wa fasihi isipotazamwa kwa jicho la tahadhari, kuna uwezekano mkubwa wa kupoteza utambulisho halisi wa utamaduni wa Mtanzania kupitia uwasilishaji wa video za nyimbo za kizazi kipya. Makala hii imechochewa na haja ya kutaka kuondosha au/na kupunguza tatizo la kukithiri kwa U-Nigeria katika fasihi. Hivyo, kwa umahususi, makala inaangazia miktadha iliyoambatana na U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili.

**Nadharia ya Utafiti**

Data za utafiti uliozaa makala hii zilichanganuliwa kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii iliasisiwa na mwanafalsafa wa Kijerumani, Gustave Flaubert (1821 - 1880). Mojawapo ya malengo ya Nadharia ya Uhalisia ni kuipinga misingi ya Nadharia ya Ulimbwende iliyoonekana kushindwa kuyatatua matatizo ya wanajamii. Msingi mkubwa aliouweka Gustave ulijielekeza katika fikra za mtu na ubainishwaji wa matatizo ya kijamii katika uhalisi wake. Baadhi ya wafuasi wa nadharia hii ni Karl Marx (1818 - 1883), Maxim Gorky (1868 - 1936), na Gyorgy Lukacs (1885 - 1971). Misingi ya nadharia hii imehusisha mtazamo kwamba fasihi ni muhimu isawiri na kuelezea mambo kwa kuzingatia uhalisi wa maisha. Pia, ieleze mambo ya kihistoria yasababishayo

mabadiliko chanya kwa jamii, na itoe picha halisi ya jamii bila kuidunisha au kuitia chuku. Vilevile, fasihi ioneshe matumaini kwa mwanadamu kuweza kushinda matatizo yanayomkabili katika mazingira yake (Wafula na Njogu, 2007). Katika makala hii, Nadharia ya Uhalisia imetumiwa kufanya ulinganisho baina ya masuala yanayoonekana katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya na namna mambo yalivyo katika jamii. Utumiaji wa Nadharia ya Uhalisia umetusaidia kuimakinikia miktadha inayorejelea uchotarishaji wa tajriba na tamaduni za Kitanzania pamoja na zile za Kinigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

**Methodolojia**

Utafiti huu ni wa kitaamuli. Hivyo, tafakuri ilikuwa ni kiini katika kuhusisha na kutoa majawabu ya taarifa kuhusu suala linalochunguzwa (Dawson, 2002). Uchunguzi ulifanyika kwa kuzingatia maoni ya watafitiwa sambamba na namna yao ya kuufahamu ulimwengu kulingana na uzoefu halisi wa maisha yao (Cresswell, 2012). Aidha, data zilikusanywa kwa njia ya kuwahoji watafitiwa 50 waliopatikana kwa njia ya usampulishaji lengwa wa kipekee, kimtajo, na wa kifursa. Watafitiwa walipatikana kwa kuzingatia maarifa na taarifa kuhusiana na mada tuliyoizamia. Waligawanywa kiuwakilishi kuanzia watazamaji, wasanii wa muziki, watayarishaji wa muziki, wanafunzi wa masomo ya fasihi ya Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Dodoma, na wataalamu wa uga wa fasihi. Mahojiano yaliendeshwa katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma. Majiji haya yalichaguliwa kutokana na kuchagizwa na ufanyikaji wa shughuli za tasnia ya muziki pamoja na upatikanaji wa wasanii wa muziki wa kizazi kipya. Watafitiwa walihojiwa kuhusu miktadha ya matumizi ya U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Pia, ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kutumia njia ya utazamaji wa video. Utazamaji

ulihusisha video 22 za nyimbo za muziki wa kizazi kipya za nchini Tanzania. Video za nyimbo hizo ziliteuliwa kutokana na kuonesha viashirio vya kubeba U-Nigeria kupitia mavazi, mitindo ya uchezaji, lugha, mtiririko wa uimbaji, na utumiwaji wa mandhari.

**Matokeo ya Utafiti**

Katika kipengele hiki, tumejadili miktadha inayowasukuma wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kutumia U-Nigeria kuunda video za nyimbo zao. Kwa ujumla, matokeo haya yameonesha kuwa matumizi ya U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kipya wa Kiswahili nchini Tanzania yamechochewa na miktadha ya namna saba ambayo ni: mivuto ya kiubidhaishaji, mivuto kutoka vyombo vya habari vya Kitanzania, mivuto ya kiujumi na kibunifu, mivuto kutoka mwigo wa wasanii nguli, mivuto kutoka misukumo ya wasikilizaji na watazamaji, mivuto kutokana na ukosefu wa alama ya utambulisho wa kitamaduni nchini Tanzania, na mivuto kutokana na ukosefu wa elimu ya kimuziki.

**Mivuto ya kiubidhaishaji**

Soko la muziki wa nchini Tanzania, mwanzoni, lilikuwa limeshikiliwa na wanamuziki wa kizazi kipya wa Kiswahili (Kasiga, 2022). Katika kipindi hicho, soko lao kubwa lilikuwa likitegemea mauzo ya muziki kupitia makampuni ya usambazaji wa muziki (Mangesho, 2003). Muziki huo ulisambazwa na kuuzwa ndani ya Tanzania na nchi za jirani. Nchi jirani zilizokuwa zikipokea muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili zilikuwa Kenya, Rwanda, na Burundi. Katika nchi ya Uganda, muziki kutoka Tanzania haukupata nafasi kubwa ya kushika soko la nchi hiyo kutokana na muziki huu kuwa na matumizi makubwa ya lugha ya Kiswahili. Uganda ilikuwa

imewekeza sana katika lugha ya Kiganda pamoja na matumizi ya lugha nyingine za kiasili (Kiango, 2002; Haonga, 2021).

Data zinaonesha kuwa, kadiri maendeleo ya sayansi na teknolojia yalivyokuwa yakipiga hatua, ndivyo fursa za kutafuta masoko mapya zilivyozidi kuongezeka. Jambo hili lilidhihirika zaidi kupitia mitandao ya kijamii. Kimsingi, kupata nafasi ya muziki wa kileo kufikika kupitia mitandao ya kijamii, kuliibua soko jipya la muziki kidunia. Nyimbo nyingi zilizokuwa zikienda pamoja na muziki, video zake zikaanza kuchukua nafasi katika mitandao ya kijamii. Hivyo, muziki wa Kinigeria ukawa wa mwanzo kuwania fursa ya kiteknolojia kwa kiwango kikubwa. Wasanii wa Kinigeria kama vile Davido, P-Square, na 2 Face Idibia wakawa maarufu katika soko la muziki wa Kiafrika na kuwaongezea kipato. Uwekezaji mkubwa ukawa umefanyika kupitia wawekezaji wakubwa wa muziki wa Kinigeria ndani ya nchi yao na katika nchi za ughaibuni walizokuwapo (Adeleji, 2016). Uwekezaji huu ulienda sambamba na uanzishwaji wa makampuni ya kurekodi muziki wa Kinigeria ambayo yalikuwa na nguvu kubwa ya kiteknolojia kuwezesha video zao kupata nguvu ya kufikika kimtandao.

Katika kushadidia hoja hii, Kayuni (2021)[1] anasema kuwa:

> Utandawazi ambao umeletwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, umewasukuma wasanii kutumia mitindo ya Kiafrika Magharibi kutokana na usambazwaji wa taarifa kwa haraka na urejeshwaji wa mapokeo ya taarifa hizo papo kwa papo. Mfano, zamani hakukuwa na mitandao ya kijamii, hivyo muziki ilikuwa ni lazima kuusikia kwa njia za redio, televisheni au kwenye majukwaa. Lakini

[1] Fortunate Kayuni ni shabiki wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Mahojiano haya yalifanyika Ubungo jijini Dar es Salaam, Januari 12, 2021.

> hali ya sasa ni tofauti. Msanii hana ulazima wa kwenda redioni ili kuachia wimbo wake. Anaweza kutumia mitandao ya kijamii kupeleka kazi yake na akapata mrejesho kutoka kwa mashabiki wake moja kwa moja. Hali hii imechangia sana wasanii kutumia mitindo ya Kinigeria kwa sababu mirejesho mingi ya kutokea kwenye mitandao ya kijamii inaonesha kuwa asilimia kubwa ya watu wanapenda kutazama video zenye mitindo ya Kinigeria kupitia *post* [andiko la kimtandao] zilizopo kwenye akaunti zao… (Ufafanuzi katika mabano mraba ni wa mwandishi).

Matokeo yameonesha kuwa, baada ya wadau wa muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria kufanya uwekezaji mkubwa wa kimtandao na kuutumia utandawazi, muziki wao ulipata mzunguko mkubwa katika vituo vya redio na runinga katika bara la Afrika. Mzunguko huo katika vituo na kumbi za starehe uliigusa tasnia ya burudani nchini Tanzania. Vituo vya redio na televisheni nchini Tanzania vikaupa muziki wa Kinigeria nafasi kubwa. Kupitia jambo hilo, wasanii wa Kinigeria wakapata fursa za kuja kufanya maonesho ya kimuziki nchini Tanzania huku wakisindikizwa na wanamuziki wa Kitanzania. Katika matamasha hayo ya kimuziki, wanamuziki wa Kinigeria wakawa wanalipwa kipato kikubwa kuliko wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kitanzania. Kutokana na hali hiyo, wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania wakasukumwa kusuka sanaa zao kwa kufuata mtindo wa Kinigeria ili kuongeza wigo na soko lao la kimuziki.

Dickson (2021) ni mmoja wa waliohojiwa na mwandishi wa makala hii kuhusu msukumo wa wasanii kutumia U-Nigeria. Anasema:

> Jambo kubwa ni kwamba Wanigeria kwa sasa wamefanikiwa sana katika muziki. Waliwanyang'anya

> tonge kinywani Waafrika Kusini na Wakongo, kisha wao wakaibuka ghafla kupitia mitandao ya kijamii. Hivyo, baada ya kushika nafasi ya kwanza katika tasnia ya muziki wa Kiafrika na kukubalika, hatimaye wameweza kugusa tuzo za *Grammy*[2] na kuzitwaa. Kwa hali hiyo, wasanii wa Kitanzania tunadhani tukitumia mtindo wa muziki wao tunaweza kwenda mbali kama muziki wao ulivyo katika soko la muziki duniani.

Kutokana na maoni ya mhojiwa huyu, ni dhahiri kwamba umaarufu wa wanamuziki na muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria umekuwa chambo kwa wanamuziki wa Tanzania kujikita katika U-Nigeria. Kupata tuzo za kimataifa kwa wasanii wa Kinigeria, pia kumekuwa ni mvuto tosha kwa wasanii wa Kitanzania kunasa katika U-Nigeria. Wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili, kisaikolojia wameingiwa na ufungwa wa kuvutwa na ladha ya muziki wa Kinigeria katika nyanja zote. Jambo hilo limewaaminisha kuwa muziki wa Kinigeria ndiyo kiwakilishi cha muziki wa Kiafrika ulimwenguni. Kupitia Nadharia ya Uhalisia, ilithibitika kuwa hali hiyo inazifanya video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya kushindwa kusawiri uhalisi wa maisha ya Watanzania. Utafiti ulibaini kuwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kitanzania wamekuwa wakiimba na kutengeneza video za nyimbo za Kinigeria kwa sababu ya nchi kukosa msingi bora wa kutunza utamaduni wao.

Akisisitiza soko kama mojawapo ya muktadha unaosababisha wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kuutumia U-Nigeria, Leyla (2021)[3] anafafanua zaidi hoja hii kwa kusema kuwa:

---

[2] Hizi ni tuzo kubwa za kimuziki duniani. Zilianzishwa mwaka 1959 nchini Marekani. Tuzo hizi zimekuwa zikitambua maeneo tofauti ya ubora katika tasnia ya muziki nchini Marekani na duniani.

[3] Leyla Issa Abdallah ni shabiki wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Mahojiano haya yalifanyika Mwenge jijini Dar es Salaam, Februari 20, 2021.

> Muziki wa Kinigeria una soko kubwa sana ukilinganisha na muziki wa nchi nyingine za Kiafrika. Muziki huu umeweza kuteka mashabiki ambao hata awali hawakuwa wakiufahamu na kuufuatilia. Utaona kuwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria walivyo na soko hapa nchini na nchi za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, kupendwa huko kumewaongezea kipato kwa kiwango kikubwa. Ukitaka kujua hilo angalia pesa wanayoingiza mitandaoni. Unafikiri wasanii wetu wataweza kuacha kitu kinachowaingizia kipato?

Maoni ya mhojiwa Leyla yanathibitisha namna wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili wasivyoweza kuacha kutumia U-Nigeria katika kazi zao. Kwao U-Nigeria umekuwa sehemu muhimu ya kuwaongezea kipato sokoni. Katika video za muziki wa kizazi kipya za Kiswahili nchini Tanzania, suala la U-Nigeria limekuwa likijitokeza kupitia mfumo wa mavazi yanayovaliwa na wasanii katika video zao, mandhari, ala na midundo inayotumika, pamoja na mitindo ya uchezaji ya wasanii. Mambo mengine yanayojitokeza katika video hizo ili kuongeza soko la muziki wao ni utumiwaji wa vifaa vya kijukwaa na matumizi ya maneno yenye asili ya Kinigeria katika video za nyimbo hizo. Maneno ya Kinigeria yaliyobainika kutumika katika video za nyimbo ni kama vile; Ifunanya, Eneka, Chineke, Shoki, Shaku, na mengine. Maneno haya yalidhihirika kupitia video za wasanii Diamond Platnumz, Marioo, Rayvanny, na Msami. Kwa kufanya hivi, wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania wamekuwa wakiamini kutazidi kuwapatia matokeo bora kibiashara.

**Mivuto kutoka vyombo vya habari vya Kitanzania**

Katika tasnia yoyote iwe ya kisanaa na kiburudani, kiuchumi na kibiashara au kijamii na kisiasa, ustawi wake hutegemea kuwapo kwa sekta ya habari (Akashraj & Pushpa, 2014; Khalid, Ahmed & Mufti, 2015; Ferrera, 2016).

Katika muziki, nafasi ya vyombo vya habari ni kubwa zaidi (Kong, 2019). Muziki huundwa ili uchezwe mahali. Kuna maeneo mbalimbali ambayo muziki hupigwa ili usikilizwe na kuchezwa. Muziki unaweza kupigwa katika kumbi za starehe mathalani kwenye nyumba za starehe zinazohusisha maonesho ya muziki. Muziki huchukua nafasi kubwa katika sherehe za kijamii kama vile harusi na mikutano ya kisiasa. Kwa kiasi kikubwa, uti wa mgongo wa utendaji wa muziki ni vyombo vya habari.

Muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria nchini Tanzania ulipata nafasi kubwa ya kupigwa na vyombo vya habari vya Kitanzania miaka ya 2007 na 2010. Kipindi hicho, video za nyimbo za wasanii P-Square za *Temptation*, *Do Me* na *Ifunyanya* zilishika chati ya vyombo vya habari nchini Tanzania. Pia, video ya wimbo wa *Fall in Love* wa D'Banj, na wimbo wa "*My African Queen*" wa 2 Face Idibia ilichukua nafasi kubwa katika vyombo vya habari vya nchini Tanzania. Kung'ara kwa muziki wa Kinigeria kukauacha pweke muziki wa kizazi kipya wa asili wa Kitanzania uliokuwa ukipigwa na wanamuziki kama vile: Dully Sykes, Ally Com, Ali Kiba, Marlaw, Z-Anto, MB Doggy na wengine (Kasiga, 2022).

Kuachwa kando na kuanza kupoteza umaarufu wao katika medali za muziki za runingani na redioni kuliwasababisha wanamuziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kuchukua mkondo mpya. Wakaanza kunukuu motifu na kufuata mtindo uliokuwa ukitamba katika vituo vya redio na televisheni. Katika kufanya hivyo, muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili ukabadilika kwa kuingiza vionjo vya muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria. Wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kitanzania ili waweze kuingia katika mzunguko wa upigwaji wa muziki wao katika vituo vya televisheni na redio wakajikuta tayari wako katika U-Nigeria. Kufanikisha jambo hilo,

msanii Diamond Platinumz akawa msanii wa kwanza kufanya ushirikiano wa kimuziki na wasanii wa Kinigeria. Mwaka 2014, Diamond Platinumz alifanya wimbo wa *My Number One Remix* aliomshirikisha mwanamuziki wa Kinigeria - Davido (Kasiga, 2022). Wimbo huo ukaingia katika mzunguko wa upingwaji katika redio za Kitanzania. Video ya wimbo huu ikawa maarufu katika vituo vya runinga. Huo ukawa mwanzo wa kuchukua kasi kwa U-Nigeria katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Katika utengenezaji wa video ya wimbo huo, ikampasa msanii Diamond Platinumz na timu ya mameneja wake wasafiri hadi nchini Nigeria ili waweze kutengeneza video ya wimbo huo. Kupitia Nadharia Uhalisia, ilibainika kuwa kuingizwa kwa U-Nigeria katika video hiyo moja kwa moja kulianza kuondoa uingizaji wa mazingira na tajriba halisi ya wasanii wa Kitanzania katika kazi zao.

Katika kukazia hoja kuhusu mivuto kutoka vyombo vya habari vya Kitanzania kama sehemu ya muktadha inayosababisha kutumiwa U-Nigeria katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili, Kayuni (2021) anasema:

> Kitu kingine kikubwa kinachochangia wasanii wetu kutumia mitindo ya Kinigeria ni vyombo vyetu vya habari. Vyombo vya habari vilivyopo nchini vimekuwa vikifanya uwekezaji wa upigaji wa muziki wa Kinigeria. Vyombo hivi pamoja na maeneo ya starehe mkazo mkubwa uko katika kupiga nyimbo za Kinigeria. Asilimia kubwa ya muziki unaopigwa ni wenye U-Nigeria badala ya kupiga nyimbo na video zenye mahadhi yetu. Kwa hiyo, ili wasanii wa muziki wa kizazi kipya waweze kupata *platform* [jukwaa la kusikika] kwenye vituo vya runinga na redio wanaamua watumie U-Nigeria kuunda sanaa yao iwe katika vipengele vyote vinavyounda video zao. (Ufafanuzi wa katika mabano mraba ni wa mwandishi).

Kama inavyoonekana katika nukuu hii, ili kuzinogesha video zao, wasanii wamekuwa wakitumia vipengele vya Kinigeria ili kazi zao zichezwe katika vituo vya televisheni vya Kitanzania. Msukumo huu umesaidia video za muziki wa kizazi kipya za Kiswahili kuweza kuingia katika kumi bora za vituo vya televisheni vya nchini Tanzania pamoja na nchi jirani. Vituo vya runinga vya *Wasafi TV*, *Clouds TV*, *TBC 1*, *ETV* na *Star TV* vina vipindi vya muziki wa kizazi kipya vinavyohusisha video za nyimbo za kizazi kipya za Tanzania, Nigeria, Afrika Kusini, na kwingineko. Jambo hilo limeongeza ushindani katika tasnia ya ndani. Vituo vingine vya Kiafrika kama vile Trace Mziki, *Magic East HD*, *Hip TV*, *Soundcity*, *Maisha Magic East HD*, na *Maisha Magic Bongo*, hivi sasa, vimeweza kuwa na kumi bora za video za Kitanzania zinazohusiha video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili zenye U-Nigeria kama kiini cha kuundia kazi hizo.

**Mivuto ya kiujumi na kibunifu**

Muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria, kwa kiasi kikubwa, umeundwa kupitia vionjo kadhaa vya kitamaduni vinavyopatikana katika nchi ya Nigeria ambayo ina zaidi ya jamii za kikanda (makabila) zipatazo 250 (Falola, 2003).  Ndani ya jamii hizo, hupatikana jamii tatu kubwa na maarufu, yaani Kiigbo, Kiyorúba, na Kihausa. Isitoshe, ndani ya jamii hizo, kuna aina nyingi ya ala na mipigo inayozalisha ladha mbalimbali katika muziki wao. Katika nchi hiyo, kumekuwa na mipango yenye kujenga ubunifu unaozalisha vitu vipya ndani ya utamaduni wake kupitia maendeleo ya sayansi na teknolojia (Anyanwu, 2019).

Kupitia andiko la Anyanwu (khj), imethibitika kuwa katika nchi ya Nigeria shughuli za kijamii na masuala ya kitamaduni ni mambo yanayodumishwa

na kushikiliwa hadi hivi sasa. Kwa mfano, tawala za kichifu bado zina nafasi kubwa ya kiutawala katika maeneo ya kiuongozi na kisiasa. Tawala hizo za kijadi huzungukwa na masuala mbalimbali ya kitamaduni yanayohusisha nyimbo na amali nyingine za kitamaduni. Kupitia Nadharia ya Uhalisia ilibainika kuwa jambo hilo limetoa nafasi kubwa kwa muziki wa Kinigeria kuwa na mahali pa kuanzia kufanyia ubunifu. Uchotaji huo wa amali za kitamaduni zilizopo ndani ya jamii zao, kumesaidia kuupa muziki wao hadhi ya kiujumi.

Katika kuthibitisha namna Wanigeria walivyo na muumamo mkubwa na tamaduni zao, Antony (2021)[4] anasema kuwa:

> Muziki wa Kinigeria wa vijana umechukua fursa ya utajiri uliomo katika muziki wao wa asili. Ifahamike kuwa jamii nzima ya Kinigeria hadi hivi sasa, bado imekumbatia shughuli za kitamaduni. Ndio maana mpaka sasa unakuta haifungwi harusi nchini Nigeria bila ya kufanyika kwanza harusi ya kijadi. Baada ya harusi ya kijadi, ndipo maharusi wataendelea na michakato ya kwenda msikitini au kanisani. Wao, harusi ya kijadi hupewa umuhimu wa kipekee. Huaminika kuwa harusi ya kijadi ndiyo yenye kutoa ithibati kwamba pande mbili za familia zimekubaliana kuibariki ndoa husika. Kwa hiyo, panapokuwa na shughuli hizi huambatana na ngoma na sanaa mbalimbali za kijadi .…

Kwa mfano, ukitazama video ya “Adda”[5] ya mwanamuziki wa Kinigeria Mr. Flavor jambo lililozungumziwa hapo juu linajitokeza. Katika video hii, inaonekana harusi ya kijadi ya jamii ya Kiigbo. Ni video ambayo wasanii

[4] Antony Asukile ni msomi wa taaluma ya muziki na mwanamuziki anayefanya kazi zake jijini Dar es salaam. Mahojiano haya yalifanyika Sinza jijini Dar es Salaam, Februari 20, 2021.
[5] https://www.youtube.com/watch?v=2lUFM8yTtUc Tazama video ya muziki wa “Adda” ya mwanamuziki wa Kinigeria Mr. Flavour.

wanaonekana wakiwa wamevaa mavazi ya Kiigbo yaliyo mashuhuri katika matukio rasmi ya jamii za Kinigeria. Katika video hiyo, wasanii wanaonekana wakiwa wamevaa mavazi hayo pamoja na vikofia vya Kiigbo vinavyoonesha mamlaka ya mtu kijamii. Kwa upande mwingine, wanamuziki wa muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria wameweza kuitumia nafasi hiyo ya vionjo vya muziki wa asili wa nchini humo kama jadi iliyoendelezwa kiteknolojia. Vionjo hivyo vimeongeza thamani ya muziki wao kwa kuitofautisha na muziki mwingine kutoka sehemu nyingine za kidunia.

Katika kulikazia suala la uibukaji wa vionjo vipya vyenye ladha kutoka utamaduni wa Kinigeria na nafasi yake katika kuunda muziki wa Kinigeria wenye ladha ya kipekee na mvuto, Leyla (2021) anasema kuwa:

> Mwanzoni muziki wa Kinigeria ulikuwa umekosa nguvu ya kiushindani katika soko la kidunia. Lakini tangu wanamuziki wake waamue kutumia utamaduni kutengeneza muziki wao, umefanya muziki wao upae. Awali muziki wa Kiafrika ulikuwa umeshikiliwa na Wakongo na Waafrika Kusini ila baada ya Wanigeria kuweza kutumia utamaduni wao, wingi wao, na teknolojia katika njia bora, wameweza kuwadondosha wote. Kutokana na matumizi yao ya amali za kitamaduni, lugha za asili na matumizi ya pijini ya lugha zao na Kiingereza, umefanya wapate muziki mzuri wa asili ulioboreshwa. Jambo hilo, limewasababisha wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kutumia mtindo wa Kinigeria ili wapate ladha ya Kiafrika katika nyimbo zao. Wameona hivi kwa kuwa ‘Bongofleva’ moja ya kitu ilijisahau ni utamaduni ….

Katika kuzidi kuiwekea mkazo hoja hii, Antony (2021) anasema kuwa:

> Nguvu kubwa kitamaduni na matumizi ya kiteknolojia iliyowekwa na wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria katika video za nyimbo zao ndiyo inawafanya wasanii wetu wa muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania kujikuta waigaji kutoka Nigeria. Vinginevyo, bado tunahitaji kuweka nguvu kubwa kwenye suala la utamaduni wetu katika tasnia …

Nukuu hii inaonesha kwamba kutokana na kutokuendelezwa kwa muziki wa asili wa Kitanzania, imekuwa ni vigumu kwa wasanii wa kizazi kipya kuchota ladha kutoka asili yao. Hivyo, wamejikuta wakivutwa kwenda kuchota vionjo vya muziki wa Kinigeria katika kunogesha tasnia yao.

**Mivuto kutoka mwigo wa wasanii nguli**

Mara nyingi, wasanii waliotangulia kufanikiwa kimuziki, huwa na athari kwa wasanii wachanga wanaochipukia. Mitindo ya muziki, uchezaji, muundo wa mashairi, mipigo, na maudhui ya muziki huakisi nyimbo za wasanii waliofanikiwa kitasnia. Kutokana na muktadha huu, imebainika kuwa nchini Tanzania, muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nao umekuwa ukiichukua sura hii katika kujijenga kwake. Mwanzoni, wasanii wa muziki huu walitumia lugha ya Kiingereza kutokana na wasanii hao kuichukua sura ya muziki wa kizazi kipya wa Marekani kama ulivyo (Omari, 2009).

Baadaye, wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kama Salehe Jabir, Mr II Sugu, na kundi la Hard Blasters waliingiza lugha ya Kiswahili katika muziki wao na kufanikisha kukubaliwa kwa muziki huu kwa jamii (Kasiga, 2022). Wasanii wengine waliochipukia katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili wakafuatia kuchukua mkondo huo. Mikondo mingine iliyopata nafasi katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania ilihusisha mitindo ya *Zouk* iliyofanywa na Banana Zorro, K-Basil,

na Bushoke. Mitindo ya *RnB* iliyofanywa na Mr. Paul, Four Crews Flavour, Rama Dee, na TID. Kisha mitindo ya kuimba mashairi ambayo yalichukua sura ya Kitanzania ikafuatia. Mitindo hiyo ilijichomoa kupitia ala na mdundo wa muziki wa taarabu na mahadhi ya kaswida. Muziki huo ukawa maarufu kwa jina la baibuda. Mitindo ya kibaibuda iliasisiwa na msanii Dully Sykes kupitia nyimbo zake za "Julietha" na "Salome". Mtindo huo ukawa maarufu kibiashara na kufanywa kwa ustadi na kundi la Daz Nundaz kupitia nyimbo zao za "Barua" na "Kamanda". Wasanii wengine waliofuatia katika mtindo huo na kupata umaarufu ni Sumalee, Ali Kiba, Diamond Platinumz, na kundi la muziki la *Two Berry* kutokea Zanzibar.

Uigaji wa mitindo ya U-Nigeria miongoni mwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya ulianza kuchipua baada ya msanii Diamond Platinumz kutoa wimbo wa *My Number One* na *My Number One Remix* alioufanya na msanii wa Kinigeria – Davido (kama ilivyofafanuliwa zaidi katika aya zilizotangulia). Kutokana na kufanikiwa kwa video za nyimbo hizo kukasababisha kila msanii anayetengeneza wimbo wake wa kizazi kipya kuanza kufuata motifu za Kinigeria. Muziki wa kizazi kipya wa aina nyingine ukaachwa. Watayarishaji wa muziki wakaacha kutumia ala za ndani za muziki kama vile singeli na mnanda katika kuukuza muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Kupitia Nadharia ya Uhalisia, inathibitika kuwa hali hiyo ilisababisha kufifisha usawiri wa maisha ya Watanzania kupitia uundwaji wa video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kitanzania.

Akisisitiza namna wasanii nguli walivyochochea mivuto ya wasanii wachanga wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania

kuutumia U-Nigeria katika kujenga muziki wao, Sanga (2021)[6] anasema kuwa:

> Kwa habari ya miktadha, naweza kusema kuwa msukumo wa kutunga na kujikuta wanatumia U-Nigeria imetokana na *influence* [mvuto] ya wasanii wakubwa wa muziki wa kizazi kipya hapa nchini. Hii ni kwa sababu suala la kutumia U-Nigeria limeanza miaka kama 9 iliyopita baada ya Diamond kushika kasi ya kisoko. Sasa wasanii wanaochipukia wanaona namna Diamond alivyofanikiwa kisoko kwa kutumia U-Nigeria. Je, wataaenda kinyume? Lazima wafuate mkondo uliopo. Wakati Diamond anauchukua U-Nigeria ku-*win global market* [kukamata soko la dunia] *automatically* [moja kwa moja] anaambukiza wasanii wengine na hivyo tunakuta tunakosa ladha ya kueleweka inayotutambulisha sisi na muziki wetu … (Ufafanuzi wa katika mabano mraba ni wa mwandishi).

Kutokana na dondoo hili, inaonesha bayana kuwa U-Nigeria katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania unachochewa na mwigo unaoletwa na wasanii nguli. Kupitia utafiti huu, imedhihirika kuwa, inapotokea msanii mashuhuri kuchukua kionjo kutoka nje na kisha kufanikiwa sokoni, basi kazi nyingine zote zitakazofuatia hujielekeza huko. Suala jingine lililobainika kuchochea mwigo wa U-Nigeria, ni la wasanii nguli wa muziki wa kizazi kipya kuwa mashabiki wa wasanii wa Kinigeria waliofanikiwa sokoni. Hivyo, ili wasanii nguli wafanikiwe katika soko la muziki, wamejikuta wakichukua vionjo, mtindo na mfululizo mzima wa muziki wa Kinigeria wa msanii wanayempenda. Hili linathibitika kupitia wimbo wa *Fall* wa Davido uliochukuliwa kama ulivyo na kutengeneza wimbo wa "Eneka" wa msanii Diamond Platinumz.

[6] Steven Sanga ni msomi wa taaluma ya muziki na mwanamuziki anayefanya kazi zake jijini Dar es Salaam. Mahojiano haya yalifanyika Sinza jijini Dar es Salaam, Februari 25, 2021.

**Mivuto kutoka misukumo ya wasikilizaji na watazamaji**

Katika tasnia ya muziki, wasikilizaji na watazamaji wa muziki huwa na maamuzi makubwa kuhusu namna ya mabadiliko ya muziki husika. Maendeleo ya sayansi na teknolojia ni kani inayoisukuma hadhira kuhitaji aina mpya ya muziki kutoka kwa wasanii wao. Aghalabu, kiteknolojia, jambo hilo huenda sanjari na fursa kwa hadhira kuweza kusikiliza na kutazama kwa kiwango kikubwa muziki ulio nje ya utamaduni wao. Wakati mwingine, jambo hili huenda sambamba na namna vyombo vya habari vinapowanyima fursa ya kusikiliza muziki wa nyumbani kwao. Kwa hali hiyo, wasikilizaji na watazamaji hujikuta kutotamani kusikia muziki wa kwao na, badala yake, wanapokea zaidi muziki wa nje. Kimsingi, hadhira inapokosa kiu ya kusikia sanaa yake, papo hapo huipunguza nguvu ya kisoko sanaa yao. Kwa hivyo, ili sanaa ya jamii iweze kukua kisoko na kimapato, hujikuta ikifuata matakwa ya kitu kinachopendwa na hadhira. Hata hivyo, kupitia Nadharia ya Uhalisia, imebainika kwamba kufanyika kwa jambo hilo huiondoa nafasi ya hadhira kujifunza mambo mbalimbali yaliyopaswa kuibuliwa na sanaa inayotakiwa kuakisi mazingira yao.

Katika tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, hadhira imekuwa na nguvu kubwa ya kuamua aina ya muziki unaotakiwa kufanywa na wasanii wa muziki wa kizazi kipya. Tangu hadhira ya muziki wa kizazi kipya ya Kiswahili ipate nafasi ya kusikiliza na kutazama muziki wa kizazi kipya kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, hadhira hii imetoa nafasi kubwa ya kuusikia muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria. Wasanii wa Kinigeria waliokuja nchini Tanzania walipatiwa mapokezi makubwa na matamasha yao kuingiza idadi kubwa ya mashabiki wa muziki tofauti na hali inavyokuwa kwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa

Kiswahili. Suala hilo likachipuza ari ya wasanii wa kizazi kipya kuona kuwa, endapo watatumia U-Nigeria kama kiunzi katika kazi zao, huenda watapata fursa kubwa ya kukua kisoko.

Katika kuiongezea nguvu hoja kuhusu miktadha inayosababisha wasanii wa muziki wa kizazi kipya kuutumia U-Nigeria katika kazi zao, Kayuni (2021) anasema kuwa:

> Wasanii wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya hapa kwetu Tanzania wanapenda kutumia mitindo ya Kinigeria sababu ya ala na midundo yao ya nyimbo ni ya kipekee. Watu wengi wanaipenda kwa sababu ni ya kuchangamsha hadhira. Wasanii wanaitumia mitindo na midundo ya Kinigeria kama kielelezo cha ubora kwenye nyimbo zao. Hili linatokana na kwamba watu wengi (mashabiki) wanapenda nyimbo za aina hiyo. Hivyo, na wao ili kuweza kushinda soko hawana budi kutumia ili waweza kupata mashabiki wanaopenda muziki wa aina hiyo ….

Nukuu hiyo inabainisha bayana kuwa uchaguzi wa aina ya muziki wa Kinigeria masikioni na machoni mwa hadhira, umetokana na upekee uliopo ndani ya muziki huo. Hata hivyo, kinachosahaulika ni kuwa upekee unaodhihirika katika muziki wa kizazi kipya wa Kinigeria ni zao kubwa la mambo mawili muhimu waliyoyafanya. Mosi, ni uwekezaji wao mkubwa uliofanyika katika uchukuaji wa ala, midundo, na namna ya kuimba kutoka katika jadi za nchi hiyo. Pili, uwekezaji wa kiteknolojia uliofanywa na Wanigeria kuupeleka muziki wao nje ya mipaka yao kumeyavuta masikio ya hadhira pana kimuziki. Hivyo basi, hadhira hususani ya Kitanzania, inataka kuona video na muziki ule wanaosikia kutoka kwa Wanigeria waupate ndani ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania.

Kwa hali hiyo, wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania wanavutwa na nguvu kubwa iliyopo mikononi mwa hadhira na, hivyo, kujikuta wanatumia U-Nigeria.

**Ukosefu wa alama ya utambulisho wa kitamaduni nchini Tanzania**

Muziki ni chombo kinachobeba, kuwasilisha, na kutoa tafsiri kuhusu utamaduni wa jamii fulani. Kitaifa, muziki ni kati ya alama bora zinazoelezea dhana nzima ya maisha ya jamii fulani inayotamba muziki wake kwa jamii nyingine zinazowazunguka. Hivyo, ili jamii iweze kutambulika vema kupitia muziki wake, ni muhimu utamaduni wake upewe nafasi katika muziki wao. Jambo hili halianzii kwenye muziki moja kwa moja. Huanza kupitia maisha ya kila siku ya jamii na namna desturi zao za kila siku zinavyoweza kurithishwa kwa kizazi kimoja hadi kingine.

Urithishaji huo huinyanyua na kuipambanua jamii kwa kuonesha idili na tunu zake mahususi na muhimu zinazopaswa kufuatwa na jamii moja kwenda nyingine. Vilevile, kupitia Nadharia ya Uhalisia, inathibitika kuwa uhalisia wa mazingira anamoishi msanii pamoja na tajriba yake, kwa kiwango kikubwa, humwathiri katika usanaji wa kazi zake. Kwa hiyo, linapokuja suala la teknolojia huwa ni jukwaa linaloboresha tamaduni za jamii husika na kuibeba kuiangaza kwa jamii nyingine ya nje. Linapofanyika jambo hilo, licha ya kuitangaza jamii yenye utamaduni husika, bado pia hutengeneza njia nyingine ya kuongeza kipato kwa wanajamii wake kupitia sanaa zinazojipambanua ndani ya utamaduni husika wa jamii hiyo.

Katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, kumekuwa na hatua ndogo za kufanya uwekezaji katika vionjo vya kiasili vya Kitanzania

katika ujenzi wa sanaa. Jambo hili limekuwa kikwazo kwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya kuhusisha utamaduni wao pindi wanapotayarisha kazi zao. Kukosekana kwa alama mahususi ya kitamaduni, kunawafanya wasanii wa muziki wa kizazi kipya wawe na jicho pana la kutazama nje ya utamaduni wao badala ya kuwa na jicho la kina la kutazama vionjo vya kitamaduni vilivyopo nchini Tanzania. Hivyo, wanajikuta wakizunguka kutafuta vionjo katika muziki wowote unaochukua nafasi ya kisoko. Hii ni tofauti na wasanii wa Kinigeria ambao wamefanikiwa kuwa na ladha ya muziki unaowatambulisha kwa kuazima vionjo ndani ya utamaduni wao. Faida yake imeweza kuonekana kwa muziki wao kushika usukani wa tasnia ya muziki wa Kiafrika kwa miaka kumi mfululizo.

Katika kueleza namna muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania unavyovutwa na U-Nigeria kutokana na ukosefu wa alama ya kitamaduni nchini Tanzania, Sanga (2021) anasema:

> Hapa nchini kwetu Tanzania hakuna urithishwaji wa tamaduni zetu kupitia malezi yetu ya kila siku. Mfano mzuri, ukitazama kizazi cha wazazi wetu asilimia kubwa wanafahamu tamaduni zao. Yaani ni wajuvi wa mila na desturi zao ikiwemo lugha za makabila zao. Jambo hilo ni tofauti kwa sisi vijana wa sasa …

Mhojiwa anaona kuwa jamii ya Kitanzania kwa asilimia kubwa, imejengwa kutokuwa na mapenzi ya dhati na utamaduni wake. Ni aghalabu kuona Watanzania wakijivunia kuongea lugha za nje ya jamii yao. Vilevile, imebainika kuwa kuna ukosefu wa ari ya kujivunia utamaduni unaopatikana katika nyimbo za asili za Tanzania. Mathalani, hakuna taratibu za kuyaenzi mavazi ya kitamaduni pamoja na mitindo yake ya kiuchezaji. Mambo hayo yangetiliwa mkazo huenda yangeuboresha muziki wa Kitanzania kwa kuupa alama ya kitamaduni inayoutambulisha kwa jamii nyingine.

Hivyo basi, kupitia utafiti, ilibainika kuwa licha ya Tanzania kuwa na jamii kati ya 125 hadi 130, bado kuna ukosefu wa alama ya kitamaduni katika sanaa zake. Video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya zimethibitisha kuwa kuna upotevu mkubwa wa mila, desturi na tamaduni za Kitanzania ndani yake. Video zimekuwa zikichukua ala na midundo, mandhari, mavazi, vifaa vya kijukwaa na chochote wanachokisikia kwa Wanigeria. Hata hivyo, wakati mwingine, vitu hivyo vimekuwa kinyume na maadili ya Watanzania. Hivyo, kuwepo kwa jambo hilo kumefifisha nafasi ya Watanzania kutambulika kupitia sanaa yao.

**Mivuto kutokana na ukosefu wa elimu ya sanaa ya muziki**

Suala la elimu ya muziki ni jambo muhimu katika ukuaji na ustawi wa tasnia yoyote. Vivyo hivyo, katika tasnia ya muziki wa kizazi kipya, suala la ufanisi wa kifani na kibiashara hutegemea uwekezaji mkubwa wa taaluma husika ya utayarishaji wa muziki, na biashara ya muziki husika. Suala la elimu ya muziki haliishii katika vyuo vinavyotoa taaluma hiyo tu, bali ni suala linalotakiwa kuendelea kufanywa kwa njia mbalimbali kama vile warsha ili kuboresha penye udhaifu na kukuza panapoonekana kuwa pamesimama barabara.

Katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili, suala hili la elimu halijapatiwa nafasi kubwa. Licha ya wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili wengi wao kutokuwa na elimu ya muziki wanaoufanya, vilevile, wamekosa mbinu za kifani zinazowawezesha kufanya muziki wao kwa namna ambayo haitauacha uasili wao na utaifa wao (Kasiga, 2022). Kutokana na kukosekana warsha za kutosha, wasanii wamejikuta wakikosa mbinu za kufanya kazi zao kwa ubora. Jambo hilo linawasukuma kujikita katika U-

Nigeria. Kujikita huko katika U-Nigeria kunasababisha mambo matatu makubwa. Mosi, kukosekana kwa muziki wenye kutambulisha taifa; pili, kuikosesha nchi kujitambulisha zaidi kisanaa, kiujumi, kifasihi na kuongeza fursa za kipato; na tatu, kuiua fikra ya kibunifu ndani ya wasanii wake.

Katika kulisisitiza jambo hili la kukosekana kwa elimu ya kitasnia kama muktadha wa utumiwaji wa U-Nigeria katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, Sanga (2021) anasema kuwa:

> Nahisi pia wanatumia mitindo ya Kinigeria kwa sababu ya ukosefu wa elimu. Wasanii wetu kwa asilimia kubwa, mambo wanayoyafanya hawajui ni kwa namna gani yanaiathiri jamii ya Kitanzania. Mitindo ya Kinigeria wasanii wetu huwa hawaanzi nayo pindi wanapoanza fani ya muziki. Huanza na 'Bongofleva'. Wakishajulikana ndipo huchukua vionjo vya Kinigeria kwa kuamini kufanya hivyo kutaunyanyua muziki wao kimataifa. Wangekuwa na taaluma kuhusu fani yao wangejiamini ….

Kupitia maoni haya, imebainika kuwa kinachokosekana ni kufahamu kuwa hata muziki wa Kinigeria haukunyanyuka tu. Kulikuwa na mipango ya kuwaendeleza kitaaluma wasanii wake. Hili linaonekana wazi kupitia wasanii wa muziki wa Kinigeria ambao kwa kiasi kikubwa wana shahada mbalimbali kutoka vyuo vikuu. Shahada hizo za kielimu zimewapa nafasi ya kufanya muziki katika uhalisia wa maisha yao. Kwa hiyo, ilibainika kwamba, endapo nchini Tanzania kungekuwa na mipango mahususi ya kuendeleza muziki na wasanii wa kizazi kipya, kusingekuwa na uchotaji wa moja kwa moja wa vionjo vya muziki wa Kinigeria katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania.

**Mapendekezo**

Kupitia uchambuzi wa data za makala hii, ilibainika kuwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya wanatakiwa kupatiwa semina na warsha kuhusu tasnia ya muziki. Vilevile, ilithibitika kwamba, kufanyika kwa jambo hilo kutawasaidia wasanii kuepukana na U-Nigeria wakati wa kusana kazi zao. Isitoshe, inapendekezwa kwamba semina na warsha hizo zijikite kuwajenga wasanii kitasnia, kibiashara, na kiutamaduni. Hali kadhalika, maarifa ya kitasnia watakayoyapata yatawamotisha wasanii kutunga nyimbo zitakazoepuka kuchota motifu za muziki wa nchi za nje kama ulivyo. Katika warsha, wasanii wahimizwe kumakinia Fasihi Simulizi ya Kitanzania, pamoja na maonesho ya sanaa za kiasili za jamii wanazotoka. Kwa kufanya hivyo, kutawasaidia kuweza kuingiza vionjo vya kitamaduni katika muziki wao. Kimsingi, utendekaji wa jambo hili utaenda mbali zaidi na hivyo kuleta tija katika muundo mzima wa video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili.

Zaidi, elimu hii itakapotolewa kupitia warsha na madarasa maalumu itawasaidia wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kujitambua. Kujitambua ambako kutaongeza ari ya kufanya muziki wa kizazi kipya ambao hautakuwa ukiachana na mila, desturi, maadili, na tamaduni zake. Kwa kufanya hivyo, itawasaidia wasanii wa muziki wa kizazi kipya kuwa na malengo mapana kuhusu muziki wao na kufahamu matokeo ya sanaa wanayofanya kijamii na kitaifa.

**Hitimisho**

Makala hii imechunguza miktadha ya matumizi ya U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania. Matokeo yanaonesha kwamba ujitokezaji wa vipengele mbalimbali vya U-Nigeria umechochewa

na miktadha ya mivuto ya kiubidhaishaji, mivuto kutoka vyombo vya habari, mivuto ya kiujumi na kibunifu na mivuto kutoka mwigo wa wasanii nguli. Miktadha mingine iliyojadiliwa imehusisha mivuto kutoka misukumo ya wasikilizaji na watazamaji, mivuto kutokana na ukosefu wa alama ya utambulisho wa kitamaduni, na mivuto kutokana na ukosefu wa elimu ya sanaa ya muziki. Hivyo, katika ukuzaji wa tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili yenye kujikita katika utamaduni wa Kitanzania, ni muhimu wasanii wa muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania wapatiwe semina, warsha, na madarasa maalumu ya kunoa vipaji vyao. Kufanyika kwa jambo hilo, kutawawezesha kusana kazi zao kwa kuiakisi jamii yao.

**Marejeleo**

Adeleji, W. (2016). The Nigerian Music Industry: Challenges, Prospects and Possibilities in *International Journal of Recent Research in Social Sciences and Humanities (IJRRSSH)*, 3 (1), 261 - 271.

Akashraj D.P & Pushpa C.O. (2014). Role of Social Media on Development. *Merit Reseach Journal of Education and Review*, 2 (2), 015 - 018.

Anyanwu, C. (2019). Nigeria's Cultural Policy and The Needs of The Performing Arts. *International Review of Humanities Studies*, 4 (2), 717 - 727.

Cresswell, J. (2012). *Qualitative Inquiry and Research Design: Choosing Among Five Approaches (2nd ed)*. Thousand Oaks: Sage Publication.

Dawson, C. (2002). *Practical Research Method: A User-friendly Guide to Mastering Research*. Oxford: How To Books Ltd.

Falola, T. (2003). *In The Power of African Cultures*. Woodbridge, Suffolk; Rochester, NY: Boydell & Brewer.

Ferrera, E. (2016). Media as a Tool for Insitutional in Develeopment. *EDI Working Papers Series*, 610 (III) 4, 1 - 27.

Haonga E.D. (2021) Sera ya Lugha katika Nchi za Afrika Mashariki na Hadhi ya Kiswahili Ulimwenguni, *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences (RUJASS*), 7 (1), 49 - 58.

Haynes, J., & Onookome, O. (eds). (2000). *Nigerian Video Films*. Ohio: Ohio University Press and Swallow Press.

Jengo, E, Mbughuni L.A & Kandoro S.A. (Wah.) (1982). *Falsafa ya Sanaa Tanzania*. Dar es Salaam: Baraza la Sanaa la Taifa.

Kasiga, G.A. (2022). Tathimini ya U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kasiga, G.A. (2021). Athari za U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania, *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences (RUJASS*), 7 (1), 118 - 135.

Kasiga, G.A. (2013). U-Nigeria katika Filamu za Ki-Tanzania: Chanzo chake, Sababu za Kutumiwa na Athari zake kwa Wa-Tanzania, (Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Khalid, M.Z, Ahmed, A., & Mufti, S. (2015). Media and Development in Society: Continuity and Challenges, *Journal of Humanities and Social Sciences (IOSR-JHSS)*, 20 (11), 47 - 54.

Kiango, G. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki, *Swahili Forum*, IX, 143 - 154.

Kong, W. (2020). Analysis of the Influence of Mass Media on Music Communication Based on Digital Conditions, *Journal of Physics: Conference Series*, 12 - 14.

Mangesho, P. (2003). Global Cultural Trends: The Case of Hip-Hop Music in Dar es Salaam, (Unpublished M.A Dissertation), University of Dar es Salaam.

Madumulla, J.S. (1993). Mwandishi wa Riwaya ya Kiswahili na Suala la Ukweli wa Maisha, *Fasihi, Uandishi na Uchapaji: Makala ya*

*Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania*, UWAVITA: 141 - 153.

Mbunda, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEPL.

Mrikaria, S.E. (2007). Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya, *Swahili Forum,* 14: 197 - 206.

Omari, S. (2009). Tanzania Hiphop Poetry as Popular Literature, (Unpublished Ph.D. Thesis), University of Dar es Salaam.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi.* Dar es Salaam: MVP.

Wafula, R.M., na Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation.

Wanjiku, M.T. (2018). Mabadiliko ya Nafasi na Mtazamo wa Wahusika Wanaume Katika Riwaya za Said A. Mohamed: Utengano (1980) na Dunia Yao (2006), (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.